JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II

Juni, 2023

DAR ES SALAAM



Edit with WPS Office



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za Simu 0716470810

Mkuu wa Shule FLORENTINE ASSENGA

Makamu Mkuu wa Shule 0717970689

Matron/Patron 0715827994

Shule ya Sekondari KISARAWE II

S.L.P36645

Tarehe 12/06/2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….
……………………………………………..
S.L.P ……………………………………..
…………………………………………….



Edit with WPS Office

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISARAWE II HALMASHAURI YA KIGAMBONI MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …………

   Shule ya Sekondari **KISARAWE II** ipo umbali wa Kilometa 27 KUTOKA FERRY KIGAMBONI Mji wa DAR ES SALAAM Usafiri wa basi kutoka mjini STANDI YA MBEZI (MAGUFULI) hadi KIVUKONI ni MABASI YA MWENDO KASI, Baada ya kuteremka mwendo unavuka KIVUKONI (PANTON) hadi KIGAMBONI baada ya kuvuka aelekee kituo cha daladala na apande daladala za KIBADA ashuke kituo cha KIBADA STANDI YA MWASONGA, panda daladala zinazoenda MWASONGA na kuteremka kituo cha KISARAWE II SEKONDARI. Kwa wanaotokea STANDI YA MBAGALA panda DALADALA ZA MWASONGA na uteremke KISARAWE II SEKONDARI.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 13/08/2023

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi ya **Dark Grey** (KIJIVU ILIYOKOLEA) (2) za darasani na Maelezo ya mshono ni rinda boksi (*ambatisha kipande cha kitambaa na picha ya mshono);*
ii. Mashati meupe ya mikono mifupi (*2*);
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*ambatisha mshono*);
iv. Sare ya Michezo track suit za blue zenye nembo ya Shule Kwa wasichana (*1*)
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vii. Sweta (*blue 1*) ;
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **Dark Green** (kijani mkolezo) 2
ix. Tisheti (T-shirt) (*3*)



Edit with WPS Office

NB: AINA YA KITAMBAA KAMA ILIVYOONESHWA HAPO JUU YA FOMU HII IWE GRADE A

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 (counter book quire 3)
ii. **Ream Paper (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo kulingana na vipimo vilivyopo katika shule husika. 2.5 x6
v. Mashuka Jozi 2, (*pink)* blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (blue)
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, panga 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**ANGALIZO:**
Michango yote (**Tshs 80,000/=)** itumwe kwenye akaunti namba **22403300001** benki ya NMB kwa jina la akaunti **SCHOOL FUND ACCOUNT, KISARAWE II. Zingatia kuandika jina kamili la mwanafunzi na tahasusi yake unapotuma mchango wake na mwanafunzi aje na Slip ya malipo anaporipoti shuleni.**



Edit with WPS Office

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi**



Edit with WPS Office

- **kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.



Edit with WPS Office

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule FLORENTINE F. ASSENGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………….**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0716470810**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0717970689**
- **Mwandamizi Taaluma 0714252682**
- **Mwandamizi Malezi 0715827994**



Edit with WPS Office